MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

# KODI NA USHURU MBALIMBALI
## MWAKA 2023/2024



Julai, 2023

**TANZANIA REVENUE AUTHORITY**

## Dira

"Taasisi ya Mapato Inayoaminika kwa Maendeleo ya Kijamii na Kiuchumi"

## Dhamira

"Tunarahisisha na Kuimarisha Ulipaji wa kodi wa Hiari kwa Maendeleo Endelevu"

## Maudhui

"Ubora wa UtendajiUshirikishwaji wa Walipakodi Matumizi ya Mifumo Ubunifu"

## Maadili ya Msingi ya TRA

Weledi,uadilifu,uaminifu na uwajibikaji

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

# KODI NA USHURU MBALIMBALI MWAKA 2023/2024

Julai, 2023

| | A: KODI YAMAPATO | VIWANGO | |
|---|---|---|---|
| Na. | MAELEZO | WAKAZI | WASIO WAKAZI |
| 1.0 | Kodi ya Kampuni: | | |
| (a) | Kodi kwenye mapato ya kampuni | 30% | 30% |
| (b) | Makampuni yanayopata hasara kwa miaka 3 mfululizo. Isipokuwa kampuni zinazo-fanya shughuli za kilimo, na utoaji wa huduma za afya na elimu | 0.5% ya mauzo ya mwaka | Hakuna |
| (c) | Kampuni mpya iliyoorodheshwa kwenye soko la mitaji la Dar es Salaam na kumilikiwa na umma kwa 30% au zaidi katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo toka tarehe ya kuorodheshwa kwenye soko hilo. | 25% | 25% |
| (d) | Kampuni mpya iliyoanzishwa kwa ajili ya kuunganisha magari, matrekta, boti za uvuvi au injini ya nje ya boti yenye Makubaliano ya kiutendaji na serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Kipindi cha miaka 5 ya mwanzo tangu kuanza uzalishaji. | 10% | Hakuna |
| (e) | kampuni mpya inayotengeneza madawa ya binadamu au bidhaa za ngozi na yenye makubaliano na serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Kipindi cha miaka 5 ya mwanzo tangu kuanza uzalishaji. | 20% | Hakuna |
| (f) | Kodi kwenye mapato ya Tawi la Kampuni ya nje ya nchi lenye ukazi wa muda mrefu. | Hakuna | 30% |

| | | | |
|---|---|---|---|
| (h) | Kodi kwenye mapato yanayorejeshwa nje ya nchi na tawi linalomilikiwa na mtu asiye mkazi. | Hakuna | 10% |
| (g) | Kodi ya mapato kwenye huduma za kimtandao | Hakuna | 2% |

| 2.0 | Kodi ya Zuio: | | |
|---|---|---|---|
| (a) | (i). Gawio la hisa kutoka kampuni zilizoorodheshwa kwenye soko la hisa la Dar-es-Salaam | 5% | 5% |
| | (ii). Gawio la hisa kutoka Kampuni mkazi kwenda kampuni nyingine mkazi ambayo inamiliki hisa 25% au zaidi | 5% | Hakuna |
| (b) | Gawio la hisa kutoka kwenye makampuni mengine. | 10% | 10% |
| (c) | Malipo ya kamisheni kwa wakala kwa kutumia fedha kwa njia ya simu za mikononi | 10% | Hakuna |
| | Ada, malipo mengine na malipo ya kamisheni kwa wakala wa shughuli za benki na malipo ya mitandao | 10% | Hakuna |
| (d) | (i) Malipo ya Riba | 10% | 10% |
| | (ii) Riba iliyolipwa kutokana na dhamana ya serikali yenye miaka isiyopungua mitatu tangu ilipo orodheshwa kwenye soko la hisa Dar es Salaam | hakuna | Hakuna |
| | (iii) Riba iliyotokana na bondi za taasisi au halmashauri ambayo imesajiliwa na zinatolewa na Soko la Hisa la Dar es salaam | Hakuna | Hakuna |
| (e) | Huduma za kiutawala na kiufundi (Uchimbaji madini, mafuta na gesi) | 5% | 15% |
| (f) | Ushafirishaji (Ndege za kukodi kwa wasio wakaazi) | Hakuna | 5% |

| | | | |
|---|---|---|---|
| (g) | Malipo ya ukodishaji Ardhi au majengo kwa ajili ya biashara | 10% | 20% |
| | Malipo ya ukodishaji Ndege | 10% | 15% |
| | Malipo ya ukodishaji Mali zingine | Hakuna | 15% |
| (h) | Ushafirishaji nje ya nchi | Hakuna | 5% |
| (i) | Malipo ya Bima yaliyolipwa na mkaazi kwa mtu asiye mkaazi | 5% | Hakuna |
| (j) | Malipo kwa ajili ya matumizi ya maliasili | 15% | 15% |
| (k) | Malipo ya Huduma za Kitaalamu | 5% | 15% |
| (l) | Malipo kwa wakurugenzi(Wakurugenzi wasio fanya kazi kwenye kampuni muda wote) | 15% | 15% |
| (m) | Malipo ya bidhaa yaliouzwa Serikalini au taasisi inayofadhiliwa na Serikali | 2% mauzo ghafi | Hakuna |
| (n) | Malipo ya Faida itokanayo na Mkopo Mbadala unatolewa na Benki iliyoidhinishwa na Benki Kuu ya Tanzania | 10% | 10% |
| (o) | Malipo ya Mrahaba utokanao na kibali au matumizi ya sinema au vifaa vyake | 10% | 10% |
| (p) | Malipo ya kwa ajili ya manunuzi ya madini ya Metali za thamani kubwa, na malipo kwa manunuzi ya aina zote ya madini ya Vito,kutoka kwa wachimbaji wadogo au wamiliki wa Primary Mining licence (PML) | 2% | Hakuna |
| (q) | Malipo kwa waliliki wa misitu iliyothibitishwa kwamba inapunguza hewa ya ukaa | 10% | Hakuna |

| 3.0 | Uwasilishaji wa Ritani ya Kodi ya zuio |
|---|---|
| | Uwasilishaji wa ritani na malipo ya kodi ya zuio hufanyika siku 7 baada ya mwezi wa makato. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **4.0** | **Pato litokanalo na uuzaji wa rasilimali** | | |
| | a) Ardhi na Majengo | | |
| | (i) Uuzaji ardhi au majengo ambayo muuzaji anazo kumbukumbu za gharama alizoingia, ukokotoaji wa kodi utafanywa kwa kutegemea.na ziada aliyopata katika mauzo husika. | 10% | 20% |
| | (ii) Uuzaji ardhi au majengo ambayo muuzaji hana kumbukumbu za gharama alizoingia, ukokotoaji wa kodi utafanywa kwa kutegemea. kiasi kikubwa kati ya bei waliyouziana au thamani iliyothibitishwa. | 3% | Haitumiki |
| | (b) Pato la ziada litokanalo na uuzwaji wa haki miliki ya Vitalu vya machimbo ya Mafuta au machimbo ya Madini | 30% | 30% |
| | (c) Pato la ziada litokanalo na uuzwaji wa Hisa au dhamana zinazomilikiwa na mtu kwenye Kampuni mkazi | 10% | 20% |
| | **Misamaha katika mauzo ya rasilimali:** | | |
| | a) Makazi binafsi yanayomilikiwa na kuishi kwa miaka miaka mitatu au zaidi na faida ya uuzaji ni shilingi milioni 15 au pungufu.<br>b) Ardhi iliyotumika kwenye kilimo kwa kipindi cha miaka miwili ndani ya miaka mitatu kabla ya uuzwaji wa ardhi hiyo na Thamani ya soko ya ardhi hiyo ni chini ya shilingi milioni 10.<br>c) Hisa zilizoorodheshwa kwenye soko la hisa la Dar-es-Salaam zinazomilikiwa na mkazi au asiye mkazi kwa kiwango kisichozidi 25%.<br>d) Kutokana na kuhamisha umiliki au hisa au taarifa za madini kwa Wabia ambao ni mwekezaji na Serikali. | | |
| **5.0** | **Mapato ya mkupuo mmoja** | | |
| (a) | Usafirishaji nje ya nchi (Kwa wasio wakazi na wakodishaji wa ndege wasio na makazi maalum nchini ) | Hakuna | 5% |
| (b) | **Msamaha wa kodi kwa mapato ya mkupuo mmoja.**<br>Mapato ya mkupuo mmoja yanayotokana na usafirishaji wa samaki, usafirishaji wa maua na mboga kwa ndege ya kigeni. | | |

| 6 | Viwango vya kodi ya mapato kwa mtu binafsi mkaazi anaejihusisha na usafirishaji wa abiria na mzigo | Viwango Vya Kodi kwa Shilingi |
|---|---|---|
| | Aina za Vyombo vya Moto | |
| | **Daraja A : Magari ya Abiria** | |
| | Yenye uwezo wa kubeba abiria hadi 15 | 250,000 |
| | Yenye uwezo wa kubeba abiria 16 hadi 25 | 550,000 |
| | Yenye uwezo wa kubeba abiria 26 hadi 45 | 1,100,000 |
| | Yenye uwezo wa kubeba abiria 46 hadi 65 | 1,600,000 |
| | Yenye uwezo wa kubeba abiria Zaidi ya 65 | 2,200,000 |
| | | |
| | **Daraja B : Magari ya Utalii** | |
| | Yenye uwezo wa kubeba watalii hadi 15 | 650,000 |
| | Yenye uwezo wa kubeba watalii 16 hadi 25 | 900,000 |
| | Yenye uwezo wa kubeba watalii 26 hadi 45 | 1,300,000 |
| | Yenye uwezo wa kubeba watalii 46 hadi 65 | 1,800,000 |
| | Yenye uwezo wa kubeba watalii Zaidi ya 65 | 2,400,000 |
| | | |
| | **Daraja C : Magari ya Mizigo** | |
| | Uzito chini ya tani 1 | 250,000 |
| | Uzito tani 1-5 | 500,000 |
| | Uzito tani 6-10 | 750,000 |
| | Uzito tani 11-15 | 1,100,000 |
| | Uzito tani 16-20 | 1,300,000 |
| | Uzito tani 21-25 | 1,650,000 |
| | Uzito tani 26-30 | 1,900,000 |
| | Zaidi ya uzito wa tani 30 | 2,200,000 |
| | **Daraja D: Vyombo vya moto kwa ajili ya ukodishaji binafsi** | |
| | Pikipiki ya Miguu miwili | 65,000 |
| | Pikipiki ya Miguu mitatu | 120,000 |
| | Teksi | 180,000 |
| | Kukodi kwa mtandao “Ride Hailing” mfano huduma za Uber au Bolt | 350,000 |
| | Kukodi huduma ya usafiri kwa pamoja (Ride Sharing) | 450,000 |
| | Huduma maalumu ya kukodi (Special hire) | 750,000 |

| 7.0 | Kodi ya Mapato ya mtu binafsi (Tanzania Bara na Zanzibar) | |
|---|---|---|
| | **Mapato kwa Mwezi** | **Kiwango cha Kodi** |
| | Mapato yasiyozidi Sh.270,000 | Hakuna Kodi |
| | Mapato yanayozidi Sh.270,000 lakini hayazidi Sh. 520,000 | 8% ya mapato yanayozidi sh. 270,000 |
| | Mapato yanayozidi Sh. 520,000 lakini hayazidi Sh. 760,000 | Sh.20,000 + 20% ya mapato yanayozidi Sh.520,000 |
| | Mapato yanayozidi Sh. 760,000 lakini hayazidi Sh. 1,000,000 | Sh.68,000 + 25% ya mapato yanayozidi Sh760,000 |
| | Mapato yanayozidi Sh.1,000,000 | Sh.128,000 + 30% ya mapato yanayozidi Sh. 1,000,000 |

**Zingatia**

1. Mapato ya mwaka chini ya shilingi 3,240,000 hayatatozwa kodi.

2. Mfanyakazi anayechangia kulingana na kifungu namba 12 cha Sheria ya Mfuko wa Elimu ya mwaka 2001, mchango huo unaweza kusamehewa kodi endapo maombi yatatumwa kwa Kamishna na kuthibitishwa.

3. Malipo ya kodi kutokana na ajira kwa mtu asiye mkazi

(i) Ujira kwa wafanyakazi wasio wakazi walio ajiriwa hutozwa kodi ya zuio ya 15%.

(ii) Jumla ya mapato yapatikanayo nchini kwa mtu binafsi asiye mkazi hutozwa kodi kwa kiwango cha 30%.

3. Wafanyakazi wenye ajira ya ziada watakatwa Kodi ya zuio itokanayo na ajira ya ziada kiwango cha 30%

4. Mfanyabiashara Mkazi ambaye ana biashara au uwekezaji Tanzania bara na Zanzibar anaweza kuomba kurejeshewa kodi aliyolipa upande mmoja katika mwaka husika wa mapato sehemu aliyojisajili.

| 7.1 | **Kodi kwenye Marupurupu ya ajira** |
|---|---|
| (a) | **Manufaa yatokanayo na matumizi ya nyumba ya Mwajiri**<br>Ukokotoaji wa marupurupu ya mwajiriwa kutokana nanyumba aliyopewa na mwajiri yatazingatia bei ambayo ni ndogo kati ya bei ya soko na ile inayozidi yafuatayo:<br>i. 15% ya mapato yote ya ajira ya mwaka ya mwajiriwa na<br>ii. Madai ya marejesho yanayodaiwa na mwajiri kutokana na kodi ya pango |
| (b) | **Manufaa yatokanayo na matumizi ya Gari la mwajiri:**<br>Manufaa yatokanayo na matumizi ya gari la mwajiri hukokotololewa kutegemeana na uwezo wa injini ya gari pamoja na umri wa gari husika kulingana viwango vilivyowekwa katika jedwali lifuatalo:- |

| | Uwezo wa injini ya gari | Lisilozidi miaka 5 | Linalozidi miaka 5 |
|---|---|---|---|
| | Usiozidi 1000c.c | 250,000/= | 125,000/= |
| | Unaozidi 1000c.c na usiozidi 2000c.c | 500,000/= | 250,000/= |
| | Unaozidi 2000c.c na usiozidi 3000c.c | 1,000,000/= | 500,000/= |
| | Unaozidi 3000c.c | 1,500,000/= | 750,000/= |

**Zingatia**

- Marupurupu haya hayatozwi kodi pale ambapo mwajiri hana madai ya makato kutokana na umiliki, matengenezo au matumizi ya gari husika.
- Bei ya soko itatumika kukadiria marupurupu ya aina nyingine.
- Ritani na malipo ya kila mwezi ya mapato yatokanayo na Ajira huwasilishwa ndani ya siku saba (7) baada ya mwezi wa malipo ya mapato ya ajira husika kuisha.

| 8.0 | Tozo ya uendelezaji Ufundi Stadi (SDL) |
|---|---|
| | i. Tanzania Bara: kiwango ni 3.5 % ya malipo yote aliyolipa mwajiri kwa wafanyakazi pamoja na vibarua kuanzia 10 kwenye mwezi husika. Mwajiri anapaswa kuwa na wafanyakazi kuanzia 10 ndipo atawajibia kulipa kodi hii.<br>ii. Tanzania Zanzibar: kiwango ni 4% ya malipo yote wanayolipwa wafanyakazi pamoja na vibarua kuanzia wa nne(4) au zaidi.<br>iii. Ritani itawasilishwa tu na mwajiri mwenye sifa ya kulipa SDL.<br><br>**TAASISI ZINAZOSAMEHEWA SDL**<br><br>a) Idara au Taasisi za Serikali ambazo zinaendeshwa kwaruzuku ya Serikali<br>b) Ofisi za Kidiplomasia<br>c) Umoja wa Mataifa na Taasisi zake<br>d) Taasisi za Kimataifa na Taasisi za Nje zinazotoa misaadaa mbazo hazijihusishi na biashara kwa namna yoyote ile.<br>e) Taasisi za dini ambazo waajiriwa wake wameajiriwa kwa ajili ya kuendesha sehemu za kuabudu, kutoa mafunzo ya dini au kuelimisha dini kwa ujumla na kutoa huduma za afya.<br>f) Mashirika yanayotoa misaada ya hiari yasiyojihusisha na biashara kwa namna yoyote ile<br>g) Serikali za Mitaa<br>h) Mwajiri wa shughuli za kilimo ambaye waajiriwa wanajihusisha moja kwa moja na shughuli za kilimo pekee<br>i) Taasisi na Vyuo vya Elimu vilivyosajiliwa ikijumuisha Shule za awali, za Msingi na Sekondari, Shule za mafunzo ya Ufundi Stadi, vyuo vya ufundi, na Taasisi nyingine za Elimu ikiwa pamoja na wanafunzi walio mafunzo-kazini kupitia wakala wa ajira wa Serikali (TAESA) na taasisi zingine za elimu. |

| | |
|---|---|
| | **Zingatia**<br>• Jumla ya malipo ni majumuisho ya mshahara, malipoya likizo, likizo ya ugonjwa, malipo yoyote yanayohusiana na likizo,kamisheni, mafao, bonasi, malipo ya kujikimu, usafiri, malipo ya kujiburudisha.<br>• Msamaha kwa Zanzibar itahusishwa Taasisi au idarazilizopo kwenye kipengele (a) mpaka (d) na (g).<br>• Uwasilishwaji wa Ritani na malipo ya SDL yatafanyika ndani ya siku saba baada ya mwezi wa malipo ya wafanyakazi na vibarua. |
| **9.0** | **Viwango vya kodi ya Mapato kwa wafanyabiashara wadogo wakaazi** |

| | Mauzo kwa mwaka | Viwango vya kodi | |
|---|---|---|---|
| | | Asiyetunza Kumbukumbu | Anaetunza Kumbukumbu |
| | Mauzo yasiyozidi sh. 4,000,000/= kwa mwaka | Hakuna | Hakuna |
| | Mauzo yanayozidi sh. 4,000,000/= lakini hayazidi sh. 7,000,000/= kwa mwaka | Sh.100,000/= | 3% ya mauzo yanayozidi sh. 4,000,000/ |
| | Mauzo yanayozidi Sh. 7,000,000/= lakini hayazidi sh.11,000,0000/= kwa mwaka | Sh. 250,000/= | Sh. 90,000/= + 3% ya mauzo yanayozidi Sh. 7,000,000/= |
| | Mauzo yanayozidi Sh.11,000,000/= lakini hayazidi Sh.100,000,000/= kwa mwaka | 3.5% ya Mauzo ghafi | |

| | |
|---|---|
| | **Angalizo**<br>Viwango vya wafanybaishara wadogo havihusishi wataalam, taaluma, wakurugenzi, tasnia ya ujenzi and tasnia ya mafunzo |
| | **Zingatia**<br>1. Kusajili wafanyabiashara wadogo na watoa huduma kwenye sekta isiyo rasmi watatambuliwa na kupewa vitambulisho ambao wana mauzo ghafi yasiyozidi Sh. 4,000,000/= kwa mwaka.<br>2. Endapo mauzo ghafi kwa mwaka yanazidi Sh. 100,000,000/= utawajibika kutengeneza hesabu za mizania.<br>3. Mtu binafsi mwenye mauzo ghafi kwa mwaka kuanzia Sh.11,000,000/= anatakiwa kutoa risiti za kielektroniki.<br>4. Mlipakodi mwenye mauzo ghafi chini ya shilingi milioni 11 anatakiwa kutoa risiti ya kuandikwa kwa mkono zenye jina la muuzaji,TIN yake, Jina la mnunuzi, aina ya bidhaa na thamani yake.<br>• *Muuzaji atakayeshindwa kutoa risiti au akatoa risiti yenye thamani ya uongo atalipa faini ya kiasi kikubwa kati ya 20% ya thamani ya bidhaa au huduma au shilingi 1,500,000/=*<br>• *Mnunuzi asiyedai risiti atalipa faini ya kiasi kikubwa kati ya 20% ya kodi iliyokwepwa au shilingi 30,000/=* |

| | |
|---|---|
| **9.1** | **Uwasilishaji wa ritani na malipo ya kodi ya mapato.** |
| **(a)** | **Ritani za kodi ya mapato** |
| | 1. Taarifa ya makadirio ya kodi ya mapato.<br>i) Kwa kipindi cha mwaka wa kalenda ni kabla au mnamo tarehe 31 mwezi Machi<br>ii) Kwa wale wasio tumia mwaka wa kalenda ni mnano au kabla ya tarehe ya mwisho ya mwezi wa tatu wa mwaka wake husika.<br>2. Ritani ya mwisho ya mapato itawasilishwa ndani ya miezi 6 baada ya mwaka wa mapato kuisha. |
| (b) | **Malipo ya kodi ya mapato kwa awamu kulingana na mwaka wa kalenda**<br>i) Mnamo au kabla ya tarehe 31 mwezi Machi |
| (c) | ii) Mnamo au kabla ya tarehe 30 mwezi Juni |

| | |
|---|---|
| | iii) Mnamo au kabla ya tarehe 30 mwezi Septemba<br>iv) Mnamo au kabla ya tarehe 31 mwezi Desemba<br>**Zingatia**<br>• Malipo ya kodi kwa wasiofuata mwaka wa kalenda utakuwa siku ya mwisho ya kila robo mwaka wa mahesabu.<br>• Ucheleweshaji wa malipo ya kodi unaambatana na adhabu pamoja na riba iliyowekwa kwa mujibu wa sheria, ambapo riba hutozwa kwa viwango vilichoidhinishwa na Benki Kuu ya Tanzania kwa wakati husika. |
| (d) | **Ritani za biashara ya Mtandaoni**<br>Mtu asiye mkazi anayetoa huduma za kimtandao anawajibika kuwasilisha ritani kabla au mnamo tarehe 20 ya mwezi unaofuata baada ya mwezi wa malipo.<br>**Zingatia**<br>Mtu atakayeshindwa kuwasilisha ritani kwa wakati atapata adhabu kila mwezi au sehemu ya mwezi aliochelewa.<br>Adhabu<br>Mtu binafsi: Kiasi kikubwa kati ya 2.5% ya kiasi cha kodi au sh. 75,000/=<br>Kampuni: kiasi kikubwa kati ya 2.5% ya kiasi cha kodi au sh. 225,000/= |

| 9.2 | Ainisho la Madaraja na Viwango vya uchakavu vinavyo ruhusiwa kutolewa kila mwaka wakati wa ukokotoaji wa kodi ya mapato kwa mali inayoweza kushuka thamani | |
|---|---|---|
| **Daraja husika** | **Maelezo ya mali husika** | **Viwango Vya uchakavu kwa Mwaka** |
| **1*** | Kompyuta pamoja na vifaa vinavyohusiana na kompyuta, mashine zinazoshughulika na takwimu,vifaa/mashine zinazojiendesha zenyewe, mabasiyenye uwezo wa kubeba abiria wasiozidi 30, magari ya mizigo yanayobeba uzito chini ya tani 7, mashine nzito zinazotembea nchi kavu na zile zinazohusika na ujenzi. | 37.5% |

| | | |
|---|---|---|
| 2* | Mabasi yenye uwezo wa kubeba abiria 30 au zaidi, magari makubwa kwa ajili ya kazi maalum, matrekta na matrekta yaliyojengewa makontena, reli, garimoshi na mashine zake, meli, matishari, vyelezo, na mashine nyingine zinazojiendesha zenyewe, mitambo na mashine zake pamoja na mashine ya upepo, jenereta za umeme, na mashine za usambazaji zinazotumika katika uzalishaji au katika shughuli za madini, mitambo na mashine maalum kwa ajili ya matumizi ya jamii, na mashine au mitambo mingine kwa ajili ya umwagiliaji na mashine zake. | 25% |
| 3* | Samani za ofisi, vifaa vya ofisi na rasilimali ambazo hazikujumuishwa kwenye madaraja mengine. | 12.5% |
| 4 | (Limefutwa) | Hakuna |
| 5** | Nyumba, majengo na majenzi mengineyo ya kudumu mfano hayo yanayotumika kwa shughuli za kilimo, ufugaji au uvuvi | 20% |
| 6** | Nyumba, majengo na majenzi mengineyo ya kudumu mfano hayo;tofauti na yale yaliyotajwa kwenye daraja la tano | 5% |
| 7** | Mali zisizoshikika. | Chukua 01 gawanya kwa muda wa uhai wa mali husika kisha ikadrie kwa nusu mwaka ulio karibu |
| 8** | Mitambo na mashine ikijumuisha mashine zinazoendeshwa na upepo, majenereta ya kufua umeme, vifaa vya usambazaji vinavyotumika kwenye kilimo, mashine za kielekroniki za risiti za kodi zilizonunuliwa na wafanyabiashara ambao hawajasajiliwa kwa ajili ya kodi ya ongezeko la thamani ( VAT), vifaa vinavyotumika kwa ajili ya utaftaji na uchunguzi wa madini au nishati ya mafuta. | 100% |

## Zingatia

Iwapo gharama zilizotumika katika ununuzi wa gari ambalo uwezo wake ni kubeba mzigo usiozidi tani moja ni zaid ya shiling 30,000,000/= basi kiasi kinachozidi hizo shilingi 30,000,000 hakitatambuliwa wakati wa ukokotoaji wa uchakavu kwa gari husika.

| 9.3 | **Punguzo la Uchakavu katika rasilimali katika shughuli za madini na mafuta** | |
|---|---|---|
| | **Mwaka wa Mapato** | **Kiwango cha uchakavu** |
| | Mwaka wa Kwanza | 20% ya gharama |
| | Mwaka wa Pili | 20% ya gharama |
| | Mwaka wa Tatu | 20% ya gharama |
| | Mwaka wa Nne | 20% ya gharama |
| | Mwaka wa Tano | 20% ya gharama |

*Zingatia* 1* Uchakavu hukokotolewa kwenye thamani ya rasilimali ambayo tayari imeshapunguzwa.

*Zingatia* 2** Thamani ya rasilimali kwa mwaka wa kwanza ndio inayotumika katika kukokotoa uchakavu kila mwaka.

*Zingatia* 3 Daraja la 4 limefutwa kwa sheria ya fedha 2016.

## B. KODI ZA MLAJI

## 10. KODI YA ONGEZEKO LA THAMANI (VAT)

### 10.1 Kusajiliwa kwa ajili ya VAT

**Makundi yafuatayo ya Wafanyabiashara wanaweza kusajiliwa kwa ajili ya VAT**

i) Wale ambao matumaini yao ya kufikia kiwango cha mauzo yanayozidi Shilingi 200,000,000/= kwa mwaka yamethibitishwa.

ii) Wale ambao wamethibitika kufikia kiwango cha mauzo yanayozidi Shilingi 200,000,000/= kwa kipindi cha miezi 12 katika mwaka wa biashara unaotangulia tarehe ya kuomba usajili

iii) Wale ambao wamethibitika kufikia mauzo yaliyo nusu ya shilingi 200,000,000/= kwa kipindi cha miezi 6 kinachoishia mwisho wa mwezi uliotangulia tarehe ya kuomba kusajiliwa,

iv) Wale ambao wanafanya shuguli za kiuchumi zinazohusisha utoaji wa huduma za kitaalamu (Professional Services) ndani ya Tanzania bara.

v) Idara au Taasisi za Serikali zinazojihusisha na shughuli za kibiashara.

vi) Wale ambao biashara zao hazijaanza kuzalisha bidhaa ambazo zinatozwa VAT lakini wangependa kusajiliwa kwa ajili ya VAT ili waweze ku-credit input tax ambayo wamelipa katika manunuzi ya gharama za uanzishwaji wa Biashara husika

vii) Wale ambao wanasajiliwa VAT kwa lazima pale ambapo Kamishina Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania atakuwa na sababu za msingi za kufanya hivyo kwa ajili ya kulinda mapato ya Serikali

viii) Usajili wa VAT uliorahisishwa kwa wale ambao ni watoa huduma za kimtandao wasio Watanzania na ambao mazingira ya biashara zao hayawaruhusu kuteaua mwakilishi kwa ajili ya VAT ndani ya Tanzania. Usajili wa VAT uliorahisishwa unafanyika bila kujali kiwango cha mauzo ya mtoa huduma husika.

| 10.2 | **Viwango vya VAT** | |
|---|---|---|
| | **Maelekezo ya miamala** | **Viwango** |
| | Mauzo ya bidhaa na huduma yaliyofanyika Tanzania bara | 18% |
| | Bidhaa na huduma zilizoingizwa kutoka nje ya Nchi. | 18% |
| | Uuzaji wa bidhaa nje ya nchi na miamala mingineyo inayohusisha Nchi za nje. | 0% |
| 10.3 | **Ufafanuzi wa Miamala Inayotozwa VAT kwa kiwango cha 0%** | |
| | **Maelekezo ya miamala** | **Kiwango** |
| | 1. Mauzo ya mali isiyohamishika iliyowekezwa katika ardhi iliyo nje ya Tanzania | 0% |
| | 2. Mauzo ya bidhaa kwenda nje ya nchi au mauzo ya ndani yaliyofanywa kwa wageni-watembezi au watalii kupitia maduka yasiyotoza kodi ( Duty-free Shops) | 0% |
| | 3. Mauzo yaliyofanywa kwa mtu aliyesajiliwa kwa ajili ya VAT Zanzibar. | 0% |
| | 4. Mauzo yaliyofanyika kwa namna ya upangaji au ukodishaji kwa kipindi kinachozidi siku 30 kwa malengo kuwa kitu kilichokodishwa kitatumika nje ya Nchi. | 0% |
| | 5. Mauzo ya bidhaa au huduma yaliyofanywa kwa ajili ya matengenezo ya vitu vilivyoingizwa Nchini kwa muda (temporary importations). | 0% |
| | 6. Mauzo ya bidhaa au huduma yaliyofanywa kwa mtu asiyekuwa raia wa Tanzania kwa ajili ya matengenezo ya bidhaa zilizo chini ya uangalizi (warranty) | 0% |
| | 7. Mauzo ya bidhaa au huduma zitakazotumika kwa ajili ya kurahisisha huduma za usafiri wa kimataifa. | 0% |
| | 8. Mauzo ya huduma zilizotolewa kwa ajili ya kutumika nje ya Tanzania. | 0% |
| | 9. Mauzo ya Umeme unaotoka Tanzania bara kwenda Zanzibar. | 0% |
| | 10.Mauzo ya huduma iliyotolewa kwa ajili ya “intelectual Propert right” itakayotumika nje ya Tanzania. | 0% |
| | 11.Mauzo ya “inter-carrier Telecommunication Services” kama vile:- a) Huduma za mawasiliano kutoka kwa Kampuni Mkazi kwenda kwa Kampuni ya nje b) Mauzo ya “termination of calls” ndani ya Tanzania bara au “transmission of siginals” ndani au kupitia Tanzania Bara. | 0% |

| | | |
|---|---|---|
| | 12.Mauzo ya mafuta ya kula yaliyosafishwa kwa kiwango cha juu (Double refined Cooking Oil). Kiwango hiki cha 0% kitatumika kwa kipindi cha mwaka mmoja hadi Juni 2024 | 0% |
| | 14. Mauzo ya nguo za pamba zilizotengenezwa na Mzalishaji wa ndani kwa kutumia pamba iliyozalishwa Nchini Tanzania. Utozaji huu wa 0% ni kwa kipindi cha mwaka mmoja hadi Juni 30, 2024. | 0% |

## 10.4 Misamaha ya Kodi ya ongezeko la thamani (VAT)

### a) Msamaha maalumu wa VAT (VAT Deferment)

Msamaha huu hutolewa kwa mujibu wa kifungu cha 11 cha sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) sura 148 kwa bidhaa zilizoingizwa kutoka nje ya nchi au zilizotengenezwa hapa nchini na ambazo zilmeainishwa chini ya sura 84, 85 ana 90 ya Tarif ya bidhaa za nje zinzoingizwa katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na zile zilizoainishwa chini ya Heading 8716 pamoja na bidhaa zilizotengenezwa au kuunganishwa hapa nchini ambazo zimeainishwa chini ya H.S Code 8701.20.90 ya Tarif husika. Msamaha huu hutolewa kwa leong la kuchagiza uzalishaji wa bidhaa zinazotozwa VAT ndani ya nchi.

Hata hvyo msamaha huu maalumu wa VAT kwa upande wa bidhaa zilizoingizwa kutoka nje ya nchi utakoma kutolewa ifikapo 30 June 2026

### Vigezo vya kusitahiki kupata msamaha maalumu wa VAT (VAT Deferment)

i) Muombaji wa msamaha maalumu wa VAT lazima awe ni Mfanyabiashara aliesajiliwa kwa ajili ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ( VAT)

ii) Bidhaa au huduma zitakazo zalishwa kwa kutumia bidhaa zilizoombewa msamaha maalumu wa VAT lazima zimuwezeshe muombaji kuwa na zaid ya 90% ya mauzo ya bidhaa au huduma ambazo zinazotozwa VAT

ii) Mnufaika wa msamaha huu maalumu atasimamiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ili kuhakikisha kwamba anatumia bihaa hizo kwa ajili ya kuzalisha bidhaa nyinginezo ambazo zinazotozwa VAT kwa kipindi cha miaka 10 ambapo ndipo VAT iliyosamehewa itachukuliwa kama tayari imeshajilipa.

iv) Ikitokea mnufaika wa masamaha maalumu wa VAT ameuza au amesafiriha nje ya Nchi bidhaa zilizonufaika na msamaha maalumu wa VAT kabla ya kipindi cha miaka 10, muhusika atalazimika kulipa kiasi chote cha VAT iliyokuwa imesamehewa hapo awali pamoja na riba

### b) Misamaha ya VAT inayotolewa na Waziri wa Fedha au Kamishina Mkuu wa TRA

Misamaha hii hutolewa na Waziri wa Fedha au Kamishina Mkuu wa TRA kwa mamlaka waliyopatiwa chini ya kfungu cha 6 cha sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ( Vat) sura ya 148 Mpaka sasa takribani miamala 7 inanufaika na misamaha hii

### c) Misamaha ya VAT kwa mujibu wa sehemu ya I na sehemu ya II ya jedwari la sheria ya VAT, Sura 148.

Sehemu ya kwanza ya jedwali ya sheria ya VAT inaorodhesha takrbani miamala 32 ya bidhaa na huduma mbalimbali zilizosamehewa VAT ama inapouzwa ndani ya nchi au zinapoingizwa kutoka nje ya nchi.

Sehemu ya pili ya jedwali la sheria ya VAT inaorodhesha takribani Miamala 33 ya Bidhaa na Huduma zilizosamehewa VAT wakati tu zinapoingizwa kutoka nje ya Nchi.

## 10.5 Uwasilishaji wa Ritani ya VAT na malipo:

Ritani na malipo ya VAT hufanyika siku ya 20 ya mwezi unaofuata baada ya mwezi wa biashara.

**Zingatia**

- Endapo siku ya tarehe 20 itaangukia Jumamosi, Jumapili au Sikukuu ritani ya VAT  itawasilishwa siku ya kwanza ya kaziinayofuata Jumamosi, Jumapili au Sikukuu.
- VAT kwa bidhaa toka nje hutozwa pale tu unapoingia Tanzania bara.
- Kila mfanyabiashara aliyesajiliwa na Kodi ya Ongezeko laThamani anatakiwa kutoa risiti za kielektroniki anapouza bidhaa au huduma.

## 10.6 Usajiri wa VAT Zanzibar

Kiwango cha usajili kwa mauzo yanayotozwa VAT ni kuanzia shilingi milion 50 kwa mwaka

**Viwango vya VAT Zanzibar**

| | |
|---|---|
| Bidhaa na huduma zinazotozwa VAT | 15% |
| Uingizaji wa bidhaa na huduma toka nje kuingia Zanzibar | 15% |
| Uuzaji wa bidhaa nje ya nchi | 0% |

## 11.0 Ushuru wa Stempu

| Maelezo | Viwango |
|---|---|
| (a) Kuhamisha miliki | |
| (i) Chini ya 20,000/= | Hakuna |
| (ii) Zaidi ya 20,000/=<br>(ii) Ardhi kwa ajili ya kilim | 0.5% ya kiasi cha sh 100,000 Jumlisha 1% ya kiasi kinachozidi Sh. 100,000 |
| iii) Ardhi kwa ajili ya kilimo | 500/= |

(iv) Hati za  Nyaraka za kibiashara na kisheria, ushuru kisheria na wa stempu hutozwa katika viwango maalum mikataba vilivyoainishwa na jedwali la sheria ushuru wa stempu.

**Misamaha ya ushuru wa Stempu**

- Risiti kwenye mauzo au huduma inayohusiana na biashara
- Kuhamisha umiliki wa mali katika chombo maalum kwa madhumuni ya kutoa dhamana zinazotegemea mali hiyo.

**Zingatia**

Ushuru wa Stempu kwenye hati mbalimbali, unapaswa kulipwa ndani ya siku 30 baada ya kusainiwa.

<table>
<tr><td>12.</td><td colspan="2">Ushuru wa Forodha (import Duty)</td></tr>
<tr><td></td><td>Aina ya Bidhaa</td><td>Kiwango cha Ushuru</td></tr>
<tr><td></td><td>(i)Bidhaa za Mtaji, Malighafi zitumikazo<br>Bidhaa na dawa za hospitali, jembe la<br>Mkono na matrekata ya kilimo na Pembejeo za kilimo</td><td>0%</td></tr>
<tr><td></td><td>(ii) Bidhaa ambazo hazijakamilika</td><td>10%</td></tr>
<tr><td></td><td>(iii) Bidhaa za mlaji na zilizokamilika</td><td>25%</td></tr>
<tr><td></td><td>(iv)Bidhaa zilizo kamilika na makundi maalum ya utozwaji kodi</td><td>35%</td></tr>
<tr><td></td><td colspan="2">Baadhi ya bidhaa hutozwa ushuru zaidi ya 35% kwa lengo la kulinda viwanda vya ndani.</td></tr>
<tr><td></td><td colspan="2">Ushuru wa bidhaa (Excise duty)<br><br>A. Utangulizi<br><br>● Ushuru wa bidhaa hutozwa kwa bidhaa maalum zinazotozwa ili kulinda viwanda vya ndani, kulinda walaji na kuwa chanzo cha mapato ya Serikali.<br><br>● Mzalishaji wa bidhaa zinazotozwa ushuru wa bidhaa anapaswa ajisajili kwenye ofisi ya TRA kwa kulipa ada ya sh. 300,000/=<br><br>Uwasilishaji wa ritani<br><br>Ritani ya ushuru wa bidhaa inatakiwa kuwasilishwa siku ya mwisho ya mwezi unaofuata.<br><br>Viwango vya utozaji ushuru wa bidhaa kwa viwango maalumu vitabadilika kila baada ya miaka mitatu (3) kuanzia mwaka wa fedha wa 2023/2024.</td></tr>
</table>

| | | |
|---|---|---|
| | **B. Ushuru wa bidhaa kutokana na ukubwa wa injini ya gari husika** | |
| | **Ujazo wa injini ya gari** | **Kiwango cha ushuru** |
| | (i) Lenye ujazo wa injini chini ya 1000cc | 0% |
| | (ii)Lenye ujazo wa injini kati ya 1000cc na 2000cc | 5% |
| | (ii) Lenye ujazo wa injini unaozidi 2000 cc | 10% |
| | (iv)Magari ya kisasa yanayotumia ama gesi tu au umeme tu | 0% |
| | **C. Ushuru wa bidhaa wa uchakavu kwa magari yaliyotumika:** | |
| | i) Magari madogo ya abiria ya kawaida (Convensinal cars) na yale yenye uwezo wa kutumia nishati-mwendo zaidi ya moja,(Hybrid Cars) yenye uwezo wa kubeba abiria wasiozidi 10 na ambayo yana umri wa kuanzia miaka 8 lakini si zaidi ya miaka 10, kuanzia mwaka gari ilipotengenezwa. | 15% |
| | ii) Magari madogo ya abiria ya kawaida (Convensional cars) na yale yenye uwezo wa kutumia nishati-mwendo zaidi ya moja, (Hybrid cars) yenye uwezo wa kubeba abiria wasiozidi 10 na ambayo yana umri wa zaidi ya miaka 10 kuanzia mwaka gari ilipotengenezwa. | 30% |
| | (iii) Magari makubwa ya abiria ya kawaida (Convensional Motor vehicles) na yale yenye uwezo wa kutumia nishati-mwendo zaid ya moja (Hybrid Motor vehicles) yenye uwezo wakupakia abiria 10 au zaidi na ambayo yana umri wa zaidi ya miaka mitano,kuanzia mwaka gari husika lilipotengenezwa. | 10% |
| | (iv) Pikipiki zenye umri wa kuanzia miaka 3 na kuendelea tokea mwaka ilipo tengenezwa. | 10% |
| | **D. Uingizaji wa vipuri vya magari vilivyotumika** | |
| | Vipuri vya magari na pikipiki vilivyotumika vinatozwa ushuru wa bidhaa | 25% |

| | | |
|---|---|---|
| | **E. Ushuru wa bidhaa kwa baadhi ya huduma** | |
| | Ada au tozo zinazolipwa kwa taasisi au makampuni ya mawasiliano kwa huduma ya kuhamisha fedha | 10% |
| **14.** | **Ushuru wa barabara kwenye nishati ya mafuta kwa lita** | Sh. 513/= kwa lita |
| **15.** | **Ushuru wa mafuta ya Taa, Gesi na spiriti** | Sh. 250/= kwa lita |
| **16.** | **Tozo ya kuendeleza Utalii:** hutozwa katika bei ya chumba | 1% ya bei ya chumba bila VAT |
| **17.** | **Tozo ya kuendeleza Reli**<br>hutozwa katika gharama ya kiforodha ya kuingiza bidhaa | 1.5% ya gharama (CIF) |
| **18.** | **Tozo ya miamala ya kifedha;** Imefutwa kwa utumaji fedha, imebaki kwa utoaji wa fedha tu | Kuanzia Sh. 10 mpaka sh. 2,000 tu |
| | **Zingatia**<br>Tozo hii haitatozwa kwa vitu vilivyosamehewa chini ya Sheria ya Forodha ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004, na vitu vilivyo samehewa katika jedwali la tano la sheria husika isipokuwa bidhaa na vifaa vya famasia sura ya 30 na 90 na mbolea kama ilivyotajwa chini ya sheria ya viwango vya ushuru wa pamoja ya Afrika mashariki. | |
| **19.** | **Ushuru wa huduma za Viwanja vya Ndege** | |
| | Safari za ndani ya nchi | Sh. 10,000/- |
| | Safari za nje | Dola 40 za Marekani |

| | |
|---|---|
| **20.** | **Uwasilishaji wa Ritani:** Ritani kwa huduma itawasilishwa mnamo au kabla ya siku ya mwisho ya kazi ya mwezi unaofuata mwezi wa biashara |

| | | |
|---|---|---|
| **21.** | **Ada za huduma ya Bandari** | |
| | Kwa wasafiri wakazi | Sh. 500/- |
| | Kwa wageni wasio wakazi | Dola 5 za Marekani |
| | **Uwasilishaji wa Ritani:** Ritani kwa huduma itawasilishwa mnamo au kabla ya siku ya mwisho ya kazi ya mwezi unaofuata mwezi wa biashara | |
| | **22. Ada ya usajili wa chombo cha moto kwa mara ya kwanza hutegemea uwezo wa injini ya gari (cc)** | |
| | **Ukubwa wa Injini (cc)** | **Ada** |
| | 501 – 1500cc | Sh.200,000/= |
| | 1501 –2500cc | Sh. 250,000/= |
| | 2501 na Zaidi | Sh. 300,000/= |
| | Ada ya kusajili pikipiki | Sh. 95,000/= |
| | Ada ya usajili kwa namba Binafsi | Sh. 5,0000,000/= kwa miaka mitatu (3). |
| | Ada maalumu ya usajili ambayo kwa kutumia ni nyongezanamba ya ada ya usajili wa gari | Sh. 500,000/= |
| **23.** | **Kuhamisha umiliki wa chombo cha moto** | |
| | Ada ya gari | Sh 50,000/= |
| | Ada ya pikipiki | Sh. 27,000/= |
| | **Ada ya Nakala ya kadi (Duplicate)** | |
| | Gari | Sh. 50,000/= |
| | Pikipiki ya matairi matatu | Sh. 30,000/= |
| | Pikipiki | Sh. 20,000/=. |
| **24.** | **Leseni za Udereva** | |
| | Ada ya leseni kila baada ya miaka mitano | Sh 70,000/= |
| | Ada ya majaribio ya udereva | Sh. 3,000/= |
| | Leseni ya muda ya udereva | Sh. 10,000/= |

| | |
|---|---|
| **25.** | **Ushuru kwa bidhaa ziendazo nje ya nchi (Export Tax)** |
| | **i)** Ngozi ghafi hutozwa 80% ya thamani (FOB) au Dola ya marekani 0.52 kwa kilo kutegemea kiasi kipi ni kikubwa. Wawekezaji wanaochakata nyama kwenye EPZ wamesamehewa kulipa Kodi ya bidhaa ziendazo nje ya nchi.<br>**ii)** Ngozi chepe bluu hutozwa 10% ya thamani (FOB)<br>**iii)** Kutoza kodi kwa **30% (F.O.B) au Dola 150 ya marekani** kwa kuangalia iliyo kubwa kwenye chuma na shaba chakavu zenye HS Code **72.0 na 74.04**. |
| **26.** | **Udhibiti wa madini kusafirishwa nje ya nchi au kwa matumizi ya ndani** |
| | Haitaruhusiwa kuondosha au kusababisha usafirishaji wa madini nje ya nchi au kwa matumizi ya ndani, hadi taratibu za sheria ya madini zitakapo kuwa zimetimizwa. |
| **27.** | **Tozo kwa Korosho zisizobanguliwa** |
| | Korosho zisizobanguliwa hutozwa ushuru wa 15% kwenye thamani (FOB) au dola 160 za Marekani kwa tani kutegemea kiwango kipi ni kikubwa |
| **28.** | **Bidhaa zisizoruhusiwa kuingia hapa nchini (Prohibited Goods)** |
| | Dawa za kulevya, Vifaa vya kutengeneza gesi za machozi, Maandishi ya uchochezi, Picha za matusi, matairi ya Magari ya kubeba abiria na biashara yaliyokwisha tumika na bidhaa zingine kama zilivyoainishwa katika sheria. |
| **29.** | **Bidhaa zisizoruhusiwa kuingia hapa nchini kwa masharti ya udhibiti (Restricted Goods)** |
| | Wanyama hai, mimea, baruti, silaha, risasi, pembe za ndovu na mabaki yake pamoja na bidhaa zingine kama zilivyoainishwa katika sheria. |
| ***Bidhaa hizi zinahitaji kibali maalum kutoka Mamlaka au Taasisi husika.*** | |
| **30.** | **Ada ya mchakato wa forodha (Processing Fee)** |
| | Ada ya 0.6% hutozwa kwa ajili ya mchakato wa kuandaa nyaraka za forodha kwa kutumia thamani ya bidhaa (FOB). |

| | |
|---|---|
| **31.** | **Bidhaa zinazotoka Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na SADC** |
| | Bidhaa zinazozalishwa katika nchi Wanachama wa EAC na SADC zitatozwa ushuru kiwango cha 0% pale zinapokidhi kanuni za uasili. Kiwango hiki hakitazihusu bidhaa zinazozalishwa katika uwanda wa wazi (EPZ) na viwanda vinavyopata msamaha wa kodi. Nchi Wanachama wa EAC ni Burundi, Kenya, Rwanda, Sudan ya Kusini, Tanzania, Uganda na Jamhuri ya kidemokrasia ya Kongo . |
| | **Zingatia**:<br><br>Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zinatekeleza mfumo wa Himaya moja ya forodha lengo ikiwa ni uondoaji wa vikwazo vya biashara na kupunguza udhibiti wa mpaka wa ndani kwa bidhaa zinazohamia ndani ya Nchi Wanachama. |
| **32.** | **Maduhuli ya Serikali:-** |
| | **1. Kodi ya Majengo : Kuanzia 01/01/2024 itasimamiwa na Serikali za mitaa.**<br><br>**Maeneo ya kutoza**<br><br>**(a) Majiji, Manispaa na Halmashauri za Miji.**<br><br>(i) **Sh. 18,000/=** kwa mwaka italipwa kwa jengo la kawaida katika kiwanja chenye jengo moja linalotumika.<br><br>(ii) Kama kuna nyumba zaidi ya moja katika kiwanja kimoja kila nyumba itatozwa **Sh. 18,000/=** kwa mwaka.<br><br>**(iii) Sh. 90,000/=** kwa mwaka kwa kila sakafu ya nyumba ya ghorofa kwa maeneo ya **Majiji, Manispaa na Halmashauri za Miji.**<br><br>**(b) Halmashauri za Wilaya**<br><br>(i) **Sh. 18,000/=** kwa nyumba ya kawaida inayotumika.<br><br>(ii) Kama kuna nyumba zaidi ya moja katika kiwanja kimoja kila nyumba itatozwa Sh. **18,000/=** kwa mwaka<br><br>(iii) **Sh. 90,000/=** kwa nyumba ya ghorofa katika maeneo ya Wilaya. |

| | |
|---|---|
| | **Angalizo:**<br><br>• Endapo jengo moja linamilikiwa na watu tofauti wenyeUmiliki, kila mmoja atalipa kodi ya jengo kwa **sehemu ya jengo anayomiliki.**<br><br>• Majengo yasiyotozwa kodi ni **Kibanda cha udongo, nyumba za nyasi na makuti na nyumba za matope au udongo** au zinazofanana na hizo na zisitumike kibiashara. |
| | **33. Ushuru wa Matangazo ya Biashara kwenye Mabango;**<br>**kuanzia Julai, 2023 ushuru huu unasimamiwa na Serikali za Mitaa** |

| 34. | **A. MICHEZO YA KUBAHATISHA** | | | |
|---|---|---|---|---|
| | **1.Kasino** | | **Kiwango Kinachotumika** | **Tarehe ya Mwisho ya Kuwasilisha Ritani na Kulipa** |
| | i.) | Kasino | 18% ya mapato yote baada ya gharama | Tarehe 7 ya mwezi Unaofuata |
| | ii.) | Kasino mtandaoni | 25% ya mapato yote baada ya gharama | Tarehe 7 ya mwezi Unaofuata |
| | | **Kodi kwa Washindi** | | |
| | i.) | Washindi Casino | 12% Thamani ya ushindi | Tarehe 7 ya mwezi Unaofuata |
| | ii.) | Washindi zaidi wa Casino | 15% ya Thamani ya ushindi | Tarehe 7 ya mwezi Unaofuata |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | **B: Aina nyingine ya michezo ya kubahatisha** | | | |
| | 1. | Michezo ya kubahatisha (spot betting ) | 10% ya GGR | Tarehe 7 ya mwezi Unaofuata |
| | 2. | Michezo ya simu (sms) | 25% ya GGR | Tarehe 7 ya mwezi Unaofuata |
| | 3. | Mashine (Slot Machines) | Sh. 100,000/= kwa mashine | Tarehe 7 ya mwezi Unaofuata |
| | 4. | Bahati Nasibu ya Taifa | 20% ya GGR | Tarehe 7 ya mwezi Unaofuata |
| | 5. | Mashine (Forty Machines Sites) | 25% ya GGR | Tarehe 7 ya mwezi Unaofuata |
| | 6. | Michezo ya Komputa (Virtual Games) | 10% ya GGR | Tarehe 7 ya mwezi Unaofuata |
| | 7. | Michezo mingine chini ya Kifungu cha 51 | 10% ya GGR | Tarehe 7 ya mwezi Unaofuata |
| | | **Tozo, Ada, Mapato au malipo toka Sekta ya Utalii.**<br>TRA imepewa jukumu la kukusanya Mapato, Tozo, Ada au Malipo katika Sekta ya Utalii kuanzia 1 Julai Ada, 2020. | | |
| *35.* | | **Malipo ya marejesho ya kodi.**<br>• TRA itatathmini na kuamua kufanya marejesho au kutokufanya ndani ya siku 90 baada ya kupokea maombi yaliyowasilishwa kwa usahihi.<br>• Kamishna atalipa marejesho ya kodi ndani ya siku 14 tangu tarehe ya kufanya uamuzi.<br>• Maombi ya marejesho ya kodi iliyolipwa kwa ziada yanatakiwa kufanyika ndani ya miaka mitatu tangu tarehe ya malipo ya kodi iliyolipwa kwa ziada au tarehe ya maamuzi ya mapingamizi ya kodi yaliyotolewa na TRA au mahakama za kikodi. | | |

| 36. | Usimamizi wa Kodi |
|---|---|
| | **Usajili wa Mlipakodi**<br><br>• Kila mtanzania mwenye umri kuanzia miaka 18 anapaswa awe na namba ya utambulisho kwa mlipakodi (TIN).<br>• Mtu yeyote anayepata kipato kupitia biashara, uwekezajiau ajira anapaswa kujisajili na kupata TIN ndani ya siku 15 baada yakuanza biashara, uwekezaji au kupata ajira.<br>• Iwapo mtu amesajiliwa na kupewa Namba ya Utambulishowa Mlipakodi (TIN) kwa ajili ya biashara au uwekezaji kwa mara ya kwanza, kiasi cha kodi ya mapato kitakachokadiriwa kitaahirishwa kwa kipindi cha miezi sita tangu tarehe ya kupata TIN.<br>• Mlipakodi aliyeahirishiwa kodi atapaswa kulipa kiasikilichoahirishwa kwa awamu tatu ndani ya mwaka husika wa mapato.<br>• Endapo kodi iliyoahirishwa itapelekea kuvuka mwaka wa mapato husika, mlipakodi atalazimika kulipa kiasi chote cha kodi katika awamu ya mwisho ya mwaka wa mapato husika. |

Mlipakodi hatazuiwa kulipa kodi ya mapato aliyokadiriwa katika kipindi kilichoahirishwa endapo ataamua kulipa kwa hiari yake.

**Uwakilishi kwenye masuala yote ya kikodi**

Mlipakodi unaweza kuwakilishwa na Wakili, Mshauri wa kodi au mtu mwingine aliyeidhinishwa kwa taratibu za kisheria na Mlipakodi mwenyewe.

**Tafsiri ya mawasiliano na nyaraka**

Mlipakodi anatakiwa kuwasilisha tafsiri rasmi ya mawasiliano na nyaraka ambazo hazijaandikwa kwa lugha ya kiswahili au lugha ya kingereza.

**Mapingamizi ya kodi**

- Mlipakodi anatakiwa awasilishe taarifa zitakazo msaidia kwenye pingamizi lake la kodi ndani ya siku 30 kwenye ofisi ya TRA anayohudumiwa.
- TRA inapaswa kutoa maamuzi ya mapingamizi ya kodi ndani ya miezi sita isipofanya hivyo unaruhusiwa kukata rufaa kwenye bodi ya rufaa za kodi.

Mtu anayehifadhi taarifa zake kwa njia ya kielekroniki anapaswa awe na kanzi data ambayo TRA itaweza kuona.

Kampuni ya ujenzi inapaswa kutoa taarifa za kampuni zinazoshirikiana naye kwenye ujezni ndani ya siku 30 tangu walipoingia mkataba wa kazi hiyo ya ujenzi.

Ikiwa una sababu ya msingi unaweza kuomba msamaha wa riba na adhabu kwenye ofisi ya TRA na TRA inaweza kukufutia adhabu na riba husika.

***“Pamoja Tunajenga Taifa Letu”***

Ukiuza toa risiti, Ukinunua dai risiti



Ulipaji Kodi wa Hiari kwa Huduma Bora za Jamii.

## Ukiuza toa risiti, Ukinunua dai risiti

*Kwa Mawasiliano zaidi tafadhali*
Tembelea ofisi ya TRA iliyo karibu nawe

au

***Kituo cha Huduma kwa Wateja***
***Namba za bure:***

0800 750075
0800 780078

WhatsApp: +255 744 233333
Facebook: tratanzania
Twitter: @ tratanzania
Instagram: @ tratanzania

Barua pepe: huduma@tra.go.tz
services@tra.go.tz

Mamlaka ya Mapato Tanzania
Postcode: 28 Edward Sokoine Drive
11105 Mchafukoge
Ilala CBD

S.L.P 11491, Dar es Salaam
Simu: +255 22 211 9591- 4, +255 22 2127080
Tovuti: www.tra.go.tz

*Ukiukwaji wa maadili kwa watumishi wa TRA:*
*Piga simu +255 689 122 515 SMS: +255 689 122 516*

***Kufichua wakwepa kodi Piga simu:***
***+255 22 2137638, +255 784 210209***

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

*Kijitabu hiki hakibadilishi yaliyomo ndani ya Sheria za Kodi. Sheria za Kodi zitatumika kufafanua sehemu isiyo eleweka.*